


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**



Simu: +255-22-2112035/40
Nukushi: +255-2122617/2120486
Baruapepe: ps@moha.go.tz

9 Barabara ya
Ohio
S.L.P. 9223
11483 DAR ES
SALAAM

25 Januari, 2017

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Meja Jenerali Projest Rwegasira amefanya ziara katika Viwanda vya NIDA na Urafiki vinavyotengeneza nguo vilivyopo jijini Dar es Salaam. Lengo la ziara hii ni kuangalia ubora wa bidhaa zinazozalishwa viwandani humo kwa kuwa Wizara inategemea kuanza kuagiza vitambaa vya sare za Majeshi yaliyopo ndani ya Wizara hii kutoka viwanda vilivyopo hapa nchini.

Katika ziara hii Meja Jenerali Rwegasira aliambatana na baadhi ya maofisa wa majeshi yaliyopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi wakiwa na sampuli za aina za vitambaa wanavyohitaji kwa ajili ya sare za majeshi yaliyoko chini ya wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Uamuzi wa Ofisi ya Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuwafuata watengenezaji moja kwa moja na hivyo kuacha kutumia wazabuni kutapunguza gharama zilizokuwa zikiongezwa na mtu wa kati. Mbali ya Viwanda alivyotembelea bado atatembelea viwanda vingine vilivyopo mikoani kama vile Arusha, Mwanza na Morogoro.

Aidha viwanda vya ndani vitainuliwa kwa kuviunga mkono kwani bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya ndani zina ubora mzuri hivyo kuzifanya hata nchi za jirani mfano Kenya na Zambia kuendelea kuagiza bidhaa kutoka viwanda vya hapa nchini.

Hata hivyo, viwanda vya ndani vya kutengeneza nguo vinaweza kupewa zabuni bila upendeleo wowote kitakachoangaliwa ni ubora wa bidhaa zinazozalishwa kama zinakidhi mahitaji ya sare za majeshi yaliyopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

A handwritten signature in black ink, appearing to read 'Christina R. Mwangosi'.

Christina R. Mwangosi
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali
Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi